

Umekaribishwa hapa



Mwongozo kwa wageni

Maktaba ya Umma ya Denver hutoa nafasi za kukaribisha ambapo kila mtu ana uhuru ya kuchunguza, kujifunza, kuunda na kumiliki. Kupitia maeneo 26 katika jiji, maktaba hujenga jumuiya kwa kutoa rasilimali muhimu zinazosaidia watu kuunganisha, kukua na kustawi. Na, yote kwa bure.

KILA MTU ANAKARIBISHWA KWENYE MAKTABA

Ni kweli. Kila mtu aliye Colorado anaweza kutumia Maktaba ya Umma ya Denver bila malipo na bila kujali wapi ulizaliwa au unatembelea kwa muda kwa gani.

JE! UNAWEZA FANYA NINI KWENYE MAKTABA?

Kuna mengi unayoweza kufanya kwenye maktaba.

Unakaribishwa kwa:

- Kuazima vitabu, magazeti, sinema na muziki kuchukua nyumbani kwa wiki 1-3. Vifaa vingi vinapatikana mtandaoni.
- Kutumia kompyuta, vifaa vya uchapishaji na nakala.
- Kuuliza msaidizi za maktaba kwa msaada wa kupata habari.

- Kujifunza Kiingereza.
- Kusoma ili ufanye mtihani wa Uraia.
- Kujiunganisha na rasilimali za jamii na faida za umma.
- Kupata msaada ya kupata kazi.
- Kupata msaada ya kuanza biashara.
- Kupata rasilimali na shughuli za kujifurahisha kwa watoto.
- Kupata msaada na kazi yako ya nyumbani.
- Kwenda kwenye madarasa na kwa matukio za kufurahisha.
- Kutumia zana kama mashine za kushona, vifaa vya kurekodi, na vichapishaji vya 3D.

JE, NINAHITAJI KADI YA MAKTABLE?

Huna haja ya kuwa na kadi ya maktaba ili kuhuduria matukio na programu kama Plaza, Storytime, madarasa za kompyuta au ideaLABs. Kadi za maktaba ni bure na ni rahisi kujiandikisha! Tembelea eneo lolote la Maktaba ya Umma la Denver na kadi ya kitambulisho ulio na picha na ushahidi wa anwani. Kitambulisho cha picha kinaweza kuwa kitambulisho cha jimbo lolote, pasipoti kutoka kwa nchi yoyote, au kitambulisho ya kibalozi.



DENVER PUBLIC LIBRARY



YALE UNAWEZA AZIMA KUTOKA KWA MAKTABLEA KUTUMIA KADI:

- Vitabu na vitabu vya mtandao.
- Vitabu vya kusikiza na vitabu vya mtandao za kusikiza.
- Filamu (kwenye DVD, BluRay na kusambaza mtandaoni).
- Muziki (kwenye CD na kusambaza mtandaoni).
- Magazeti na Magazeti za Digitali.
- Magazeti za habari.
- Wi-Fi hotspots.
- Makumbusho na pasi za kuingia Hifadhi za jimbo.
- Na mengine mengi Zaidi!

MIPANGAO NA HUDUMA

Tembelea tovuti ya maktaba kwenye mtandao—denverlibrary.org—kwa habari kuhusu mipango na huduma na kupata mipango katika maeneo yote 26 ya Maktaba ya Umma ya Denver.

Plazas

Plazas ni nafasi wazi za jamii ambapo wahamiaji kutoka kote duniani wanaungana na rasilimali na kukutana na watu wapya. Shughuli zinajumuisha mazoezi ya lugha ya Kiingereza, maandalizi ya uraia, msaada wa kompyuta, sanaa na ufundi, ujenzi wa jamii na zaidi.

Rasilimali za Jamii

Kutana na mtaalamu kwa usaidizi ya kutumia rasilimali za jamii kama makazi, nyumba, chakula, faida za umma, afya za kiakili, huduma za matibabu, matibabu baada ya kutumia madawa za kulevyta, na zaidi ... uliza tu!

Wakati wa hadithi

Hadithi, nyimbo, mashairi na zaidi kwa watoto wachanga, watoto wadogo na wazazi wao au walezi waliowasilishwa kwa Kiingereza na Kihispania.

Masomo za kompyuta

Darasa na mazoezi za kibinagsi kwenye mada mbalimbali za teknolojia, kutoka kwa msingi hadi ngazi za juu, yaliyotolewa kwa Kiingereza na Kihispania.

ideaLABs

Makerspaces ni nafasi za jumuiya huru za kufanya mambo. Wazo la maktaba la ideaLAB husaidia mtu yeyote kufanya tovuti, video, michezo, muziki na zaidi. Wakati vifaa vinatofautiana kwa kila eneo, ideaLABs kwenye Maktaba ya Tawi la Gonzales ya Rodolfo "Corky" ina lenga aina za nguo: mashine za kushona, mishono na gurudumu husaidia watu kutengeneza kila aina ya vitu, ikiwa ni pamoja na nguo, quilts, sanaa za vitambaa na zaidi. Kwa kutumia vifaa vya kisasa na msaada ya wataalamu wa kiufundi, ideaLAB hutoa ufikiaji wa bure wa rasilimali ambayo inaweza kuwa haiwezekani kufikiwa. Hakuna kadi ya maktaba inahitajika.

MANENO TUNAYOTUMIA

- **Borrow or check out:** azima au jichukulie: kupeleka nyumbani kwa kipindi cha muda.
- **Due date:** tarehe ya mwisho: siku ambayo bidhaa lazima irejeshwe kwenye maktaba.
- **Items or materials:** vitu au vifaa: vitabu, sinema, muziki, na mambo mengine ambayomaktaba humiliki.
- **Librarian:** Mkutubi: mtaalamu ambaye anaweza kukusaidia kujifunza jinsi ya kutumia maktaba na jinsi ya kupata taarifa unayohitaji.
- **Library card:** kadi ya maktaba: kadi ya bure ya uanachama ambayo unahitaji kuazima vifaa kutoka kwa maktaba.
- **photo ID:** Kitambulisho cha picha: kadi ya kitambulisho inayoonyesha jina lako na picha yako. Inaweza kuwa kitambulisho ya jimbo lako, pasipoti kutoka nchi yoyote au ubalozi. Leta kile unacho na tutasaidiana kufanya kadi ya maktaba.
- **Proof of address:** ushahidi wa anwani: muswada au chochote kama anwani ya barua ulio na jina lako ikidhibitisha wapi unakoishi.
- **Receipt:** risiti: kipande cha karatasi kinachoonyesha vitu umeazima na wakati wa kurejesha.
- **renew:** Kufanya upya: ombi la kuazima vifaa kwa wakati wa ziada.
- **Return:** kurudisha: kurejesha vifaa kwenye maktaba.